**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**


**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule**
**0763401829**
**Makamu Mkuu wa Shule 0769740691**
**Patron 0652540592**
**Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda**
**S.L.P. 11 IFUNDA**

**Tarehe 01/11/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA – IRINGA 2026**

1. Tunayo furaha kukuarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda- Iringa mwaka 2026 katika mchepuo wa **AMALI**.
2. **MAAGIZO MAALUMU**.

Shule itafunguliwa tarehe **13/01/2026** KARIBU SANA. Tuna imani kuwa kwa wakati wote utakaokaa Ifunda utakuwa tayari kupokea, kujifunza, kutii na kutekeleza maagizo, sheria na taratibu za Shule ya Bweni kwa kutumia busara, hekima, utii na uaminifu mkubwa.

3. **MAZINGIRA YA SHULE KWA UFUPI**:

Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda ipo umbali wa Kilometa 45 Kutoka IRINGA mjini kwa barabara ya kwenda MBEYA. Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi Igumbilo au Ipogoro Nauli ni Tshs 2,000. kituo cha kushuka ni Ifunda shule, kwa wanaotokea barabara ya Makambako kituo cha kushuka ni Ifunda shule. Nauli ya bodaboda kutoka hapo kituo cha kushukia hadi shuleni ni Tshs. 1,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13 JANUARI 2026 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 13 JANUARI 2026

(b) Shule hii ina kidato cha Kwanza hadi cha Sita.

Kidato cha **kwanza** hadi cha **nne** ni wavulana pekee, kidato cha **tano** na **sita** ni mchanganyiko wasichana na wavulana. Wanafunzi wote hulala bwenini hivyo, kuna mabweni ya wavulana na wasichana lakini wote husoma pamoja na kula pamoja katika mabwalo ya chakula.

(c) Shule ni ya mchepuo wa AMALI YA KIHANDISI (UFUNDI) kwa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Amali zinazotolewa hapa shuleni zina sehemu kuu tano ambazo ni:

(i) ELECTRICAL INSTALLATION

(ii) SOLAR POWER INSTALLATION

(iii) PLUMBING AND PIPE FITTINGS

(iv) AUTO ELECTRICS

(v) WOOD PROCESSING

4. **MASHARTI MUHIMU NA VIFAA VYA LAZIMA:**

Kila Mwanafunzi anayejiunga na shule hii lazima aje na vitu vyote vilivyoorodheshwa hapa chini.

MAHITAJI

1. Mashati meupe ya mikono mirefu tetron mawili (2) au zaidi.

2. Viatu vya ngozi visigino vifupi rangi nyeusi vya kamba jozi mbili (2) au zaidi.(VISIWE MFUMO WA MABUTI)

3. Nguo za michezo:
   - Bukta na T- Shirt rangi ya blue masai.
   - Viatu vya michezo.
4. T- shirt ya kijivu yenye kola (form six) yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na tano.
5. T- shirt nzito zenye kola ( form six) nyekundu zinapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na tano (Tshs 15,000/= au unaweza kuja nayo)

6. Soksi rangi nyeupe jozi mbili (2)

7. Taulo, nguo za ndani za kutosha, blanketi zito, mashuka mawili (2) ya kulalia ya rangi ya bluu Bahari (moja la kujifunika na lingine la kutandika kitanda)
8. Godoro la sponji 3 x 6 (nchi nne)
9. Sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko
10. Ndoo ndogo 2 na fagio za chelewa 2 kwa ajili ya usafi binafsi
11. Mathematical set

12. Madaftari makubwa (counter book 12), msomi 12, kalamu (peni na penseli) na fedha za matumizi binafsi.

13. Ovaroli la rangi ya bluu, kofia ngumu ya kihandisi na "safety boot" kwa ajili ya masomo ya ufundi,
14. Suruali mbili (2) au zaidi rangi ya dark blue aje nazo, chini size 15 -16 inch.
15. Suruali za dark green mbili (2) aje nazo (nguo za kushindia)
16. Matibabu ya mwanafunzi anapougua ni juu ya mzazi au mlezi wa mwanafunzi

    NB : SHULE INAMSHAURI MZAZI KUMKATIA BIMA MWANAFUNZI
17. Tai moja (1) rangi ya dark blue yenye nembo ya shule.(Inapatikana shuleni)
18. Track suit nyekundu yenye mistari nyeupe pembezoni.
19. Sweta zito rangi ya bluu mshono wa (V) moja au zaidi.
20. Vitabu vya masomo atakayosoma kwa wazazi wenye uwezo.
21. Jacket zito jeusi lisilovuka magoti, lisilokuwa na maandishi, lisilokuwa na picha au kofia kwaajili ya kujikinga na baridi wakati wa maandalio ya jioni.
22. Kofia (mzula) wenye rangi ya bendera ya taifa ya Tanzania kwa ajili ya kujikinga na baridi aje nayo.

23.Rimu Mbili za karatasi kwa ajili ya matumizi ya mitihani na mazoezi ya mara kwa mara.

24. Mwanafunzi aje na faili moja (spring file) kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka zake.

25. Kamusi ya Kiingereza kwa ajili ya matumizi yake na somo la English **OXFORD/CAMBRIDGE Advanced, English learners Dictionary**.

26. Mwanafunzi aje gambuti jozi moja kwa ajili ya kazi za njee/shamba wakati wa mvua.

27. Baada ya utangulizi wa fani zote za AMALI (ufundi) mwanafunzi atatakiwa kuwa na tool box ya fani yake husika.

28. Kila mwanafunzi aje na Mswaki pamoja na dawa ya Meno, mifagio miwili ya chelewa, ndoo mbili

**ZINGATIA:**

**A. NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KUJA NAZO SHULENI:** Mwanafunzi akipatikana nazo atapewa adhabu kali hata kurudishwa nyumbani. (Kusimamishwa masomo)

**B. PIA NGUO ZA KIHUNI** zinazobana, nguo fupi au zinazoonesha maungo yake na mapambo kama vile heleni mikufu pete nk. haviruhusiwi shuleni.

**C**. Kila mwanafunzi atajigharimia **nauli** yake wakati anapokuja shuleni na wakati wa kurudi nyumbani, Shule inapofunguliwa na kufungwa.

D. Mwanafunzi anatakiwa kukamilisha ujazaji wa fomu zifuatazo kabla ya kuletwa shuleni,( zijazwe kikamilifu na kwa usahihi.)

1. Fomu ya maelezo ya Daktari (Medical Examination Form)
2. Fomu ya kukubali nafasi uliyopewa, sheria kanuni na maelekezo
3. Fomu ya kujieleza mwanafunzi mambo binafsi (Personal Particulars).
4. **KIVULI CHA CHETI CHA KUZALIWA AJE NACHO**.
5. Mwanafunzi awe na akaunti ya benki kwa ajili ya kuhifadhia fedha zake za matumizi
6***. Ni marufuku kwa mwanafunzi :***

A***. Kuja na simu shuleni,(KWA NAMNA YOYOTE ILE HAKUNA MWALIMU ANAYERUHUSIWA KUTUNZA SIMU YA MWANAFUNZI)***

B***. Kuja na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.***

...................................

**NYAHI, A. J.**

**MKUU WA SHULE**

**1. Viambatisho na Fomu Muhimu:**

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makossa ya jinai.

c) Mkataba wa mwanafunzi, mlezi/mzazi baina ya shule ya sekondari ifunda.

d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

e) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**2.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA**
**SHULE HII**

**Nakala**

1. Katibu Mkuu,
   Ofisi ya Rais,
   TAMISEMI,
   S.L.P. 1923
   **DODOMA.**

2. Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari,
   Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
   S.L.P. 9121,
   **DAR ES SALAAM**.

3. Mkurugenzi Mtendaji,
   Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,
   S.L.P. 108,
   **IRINGA**

4. Afisa Elimu (M),
   S.L.P. 858,
   **IRINGA**

5. Afisa Elimu Sekondari (W),
   S.L.P. 642,
   **IRINGA**.

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda,
S.L.P. 11,
**IFUNDA.**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla jambo la lazima.

b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c. Kushiriki kwa ukamilifu kufanya maandalio ya asubuhi, jioni na usiku (morning , evening and night preparation)

d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule g. Kuvaa sare ya shule safi wakati wote unapotakiwa.

h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

i. Kutunza mali za umma.
j. kutunza miundombinu ya shule muda wote uwapo shuleni.

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupiga, Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni .( kunyoa kwa mtindo wa panki )

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**...............................**

**NYAHI A. J.**

**MKUU WA SHULE**

**NAMBA YA SIMU:** 0763 401829

## JAZA FOMU HIZO NA KUZIRUDISHA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA**

**<u>Sehemu ya Mwanafunzi:</u>**

Mimi……………………………………….......................
Msichana/Mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ………………….................. mwaka …………........... katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda, na nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za Nchi.

Nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika katika masomo na kazi za Elimu ya Kujitegemea.

**<u>Sehemu ya Mzazi/Mlezi</u>**

Mimi. …………………………………Ninakubali mtoto wangu kuingia Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda kidato cha ………………… mwaka ………na

Ninaahidi kumpatia mahitaji yote kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule (Joining Instructions) ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni:

…………………………………………………………………
…………………………………………………………………
…………………………………………………………………
………………………………………………………………

Namba ya simu ya mkononi …………………… ya mezani/ofisini…………….

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa na Mkuu wangu wa Idara au Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata/Kijiji.

Sahihi ……………… Tarehe ………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IFUNDA**
**S.L.P. 11,**
**<u>IFUNDA</u>**

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina …………………………………………….............tarehe ya kuzaliwa……….............(taja mwaka na mwezi)
2. Kabila……………………………Taifa……………………….............
3. Dini na madhehebu ……………………………………….........
4. Jina la Baba …………………………………………………...........
5. Anwani ya Baba
……………………………………………………………............……………
……………………………………………………………......
6. Kazi ya Baba………………………………………………….................
7. Jina la Mama ………………………………….................Kazi yake
…………….......
8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana ………………………………
9. Jina na anwani ya Mlezi wako (kama si Mzazi)
………………………….......................................................................
………………………………………………………………….........
10. Wakati wa likizo utakwenda kwa nani na wapi
…………………………….............. (taja sehemu moja tu utakakokwenda kila wakati) .......................................................

11. Hapa Mkoani Iringa nina/sina ndugu …………………………….............
Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalo hapa chini.

| JINA LAKE | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI | ANWANI NA NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

12  Ninathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni kweli na sahihi
Sahihi ya Mwanafunzi ………………………..............Tarehe: ……………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……………………................. Tarehe ………………

13. Jina na sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji

………………..........................................................

Mhuri: ....................................................................

**MKATABA WA MWANAFUNZI, MZAZI /MLEZI BAINA YA SHULE YA SEKONDARI UFUNDI IFUNDA**

Mimi..............................................Mwanafunzi wa Kidato cha.............. Mwaka 20…

Ninaahidi:

1. Kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa katika Fomu ya maelekezo ya Kujiunga na Shule hii niliyojaza hapa shuleni.

2. Kuhudhuria vipindi vyote Darasani kwa kuzingatia ratiba ya shule. Kwenda kinyume na sheria hii nichukuliwe hatua za kinidhamu.

3. Kuzingatia Taaluma kwa kuweka juhudi ili kufaulu masomo vizuri kwa kuhakikisha ninapata Alama zisizopungua asilimia 75 kwa kila somo. Kupata pungufu ya alama tajwa nichukuliwe hatua za kinidhamu.

4. Kutunza na kulinda miundo mbinu yote ya shule. Kuharibu miundo mbinu hiyo nitalazimika kulipa gharama na kuitengeneza; mifano ya miundo mbinu bomba,rangi za kuta ,miundo mbinu ya umeme, vioo, madirisha, taa, dari, milango na vitasa, miundo mbinu ya vyoo, n.k.

5. Kutunza vifaa vya maabara na vitabu vya shule. Kuvunja , kuharibu na kupoteza vifaa au vitabu nitalazimika kulipa kifaa au kitabu husika.

6. Kutunza samani zote za shule. Kuharibu samani za shule nitalipa samani husika.

**7.** Kuja na Kamusi ya Kiingereza kwa ajili ya matumizi yangu binafsi-
**Oxford/Cambrige Advanced English learners Dictionary.**

8. Kutumia lugha ya kiingereza wakati wote nitakapokuwa shuleni.

9. Kutokumiliki au kutokuwa na simu ya mkononi, flash, kompyuta, Kadi ya simu, pasi ya umeme, mshumaa,kiberiti, kisu, radio, nguo zisizokuwa sare ya shule, nguo za shule zinazobana miguu hususani suruali ,sketi fupi, sketi zenye belti pana, kifaa au vifaa chochote hatarishi. Kumiliki au kuwa na chochote kati ya vitu hivi nitalazimika kulipa uharibifu wa miundo mbinu na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

10. Kukabidhi namba za Mzazi / Mlezi kwa utawala kwa ajili ya mawasiliano muhimu

11. Kutumia namba bainifu na pekee za mawasiliano shuleni:

Registrar No: 0763170327 FRIDA TWEVE
0763486398 ELIKA UVAMBE

Hizi ni njia pekee za mawasiliano nitakazotumia. Endapo nitatumia njia tofauti nipewe adhabu kali.

12. Sitajihusisha na mapenzi au kuwa na mahuasiano ya kimapenzi na mwanafunzi mwenzangu au mtu yeyote ndani au nje ya shule. Ikibainika nichukuliwe hatua za kinidhamu.

13. Kuwepo bwenini kwa wakati sahihi, kulala bwenini katika chumba nilichopangwa kila siku. Kwenda kinyume na utaratibu huu nichukuliwe hatua za kinidhamu.

14. Kuzingatia tarehe ya kufunga shule na kufungua shule kwa kutoondoka mapema kabla ya shule kufungwa na kuripoti shule tarehe ya kufungua shule. Kwenda kinyume na hili nitakosa sifa yakuendelea kusoma katika shule hii, hivyo nifukuzwe shule.

Jina la Mwanafunzi. ……………................Saini................. Tarehe........

Mzazi/Mlezi

Mimi.................................................................... Nimesoma na kuelewa yaliyoandikwa ninakubaliana na Masharti haya ambayo ni nguzo muhimu kwa ufaulu na maendeleo ya mwanangu kwa faida binafsi na Taifa kwa ujumla. Hivyo nitamwezesha mwanangu kwa hali na mali kuweza kukamilisha hayo ili kuweza kufaulu Kitaaluma.

Anwani yangu ya kudumu.

.............................................

..............................................

.................................................

Namba ya simu. ......................................... ya mkononi/Mezani/Ofisini …………………….

Nakubali haya mbele ya:-

**…………………………………**
**NYAHI A. J.**
**MKUU WA SHULE**

**PRIME MINISTER OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**
**IRINGA DISTRICT COUNCIL**

**IFUNDA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by a Medial Officer in respect of all Form I entrants)

Pupil's full name …………………………………………………….

Age ………………(years) Sex ……………………....

Blood count (Red and white) ……………………………….........

Stool Examination ………………………………………….........

Syphilis and other venereal diseases test

..........................................................................................................

T.B. Test

……………………………………………………………………

Eye Test

………………………………………………………………………

Ears

………………………………………………………………………

Spleen

………………………………………………………………………

Abdomen

…………………………………………………………………………

Urine for plamotest

……………………………………………………………………..........

Test for pregnancy (for girls only)

……………………………………………………….........

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g. physical defects, impartments e.g. am legrete)

Infections, chronic of family diseases etc
……………………………………………...........

……………………………………………………………………………
………………………

**I certify that the above is fit to pursue studies in**

**Technical Education.** Station………………………

Signature ………………………………………………. Date

………………………... Designation ……………………

**MICHEZO**



**SHAMBA DRESS**





**SARE YA DARASANI**



**TRACKSUIT**